**HALMASHAURI YA WILAYA YA MKALAMA**
**UPIMAJI WA UTAMILIFU WA KIDATO CHA PILI**
**ELIMU YA DINI YA KIISLAMU**

**Muda: Saa 2** **MEI, 2025**

**Maelekezo**

1. Mtihani huu una sehemu **A**, **B** na **C** zenye jumla ya maswali kumi (10).
2. Jibu maswali **yote** kutoka sehemu A na B na C.
3. Vifaa vya mawasiliano **haviruhusiwi** katika chumba cha mtihani.
4. Andika kwa kalamu ya wino wa bluu au mweusi.
5. Kumbuka kuandika **namba yako ya mtihani** katika kila ukurasa wa kitabu chako cha kujibia.

**SEHEMU A (Alama 15)**

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii

1. Chagua herufi ya jibu swahihi katika swali la (i) - (x) kisha andika herufi hiyo katika sehemu iliyotengwa.

(i) Aisha aliwaelimisha wanafunzi wenzake kuhusu maana ya dini kwa usahihi. Ni maelezo gani kati ya yafuatayo hayakutolewa na mwanafunzi huyo?
A. Uwezo, mamlaka au utawala
B. Itikadi inayofuatwa na watu
C. Imani ya kuwepo Allah (S.W)
D. Mfumo wa maisha ya akhera.

(ii) Mwalimu Kiboko aliwafundisha wanafunzi wake sababu za wanadamu kuomba mwongozo wa maisha kwa Allah (S.W) kwa usahihi. Ni sababu gani haikuelezwa na mwalimu huyo kati ya zifuatazo?
A. Mwanadamu ana udhaifu katika umbile lake
B. Mwanadamu ana elimu ndogo isiyotosheleza
C. Mwanadamu anaathiriwa na mazingira yake
D. Mwanadamu ni mchoyo na mbinafsi sana.

(iii) Jambo gani kati ya haya linamaanisha Sunnah kivitendo?
A. Kuonja chakula kidogo
B. Kuwapenda jamaa zako
C. Kuuza dawa za kiarabu
D. Kuvaa kanzu siku zote

(iv) Ni upi mgawanyo sahihi wa elimu kwa mujibu wa Uislamu.
A. Elimu ya Akhera na elimu Dunia
B. Elimu ya fiqhi na elimu ya tawhid
C. Elimu ya sayansi na elimu ya sheria
D. Elimu ya mwongozo na elimu ya mazingira.

(v) Mwalimu Juma aliwafundisha wanafunzi wa kidato cha pili nguzo ya tano ya Uislamu iliyosimuliwa katika hadithi mbalimbali. Bainisha nguzo hiyo kati ya nguzo zifuatazo.

A. Shahada
B. Hija
C. Swaumu
D. Zakat

(vi) Jozi ipi kati ya zifuatazo si miongoni mwa sharti za Swala?

A. Twahara na stara
B. Kuelekea Qibla na kuchunga wakati
C. Kuelekea Qibla na khushui
D. Stara na kuelekea Qibla

(vii) Maelezo yapi kati ya yafuatayo yanaonesha umuhimu wa kusimamisha swala kwa Muislamu?
A. Swala ni ibada ya kwanza kufaradhishiwa
B. Kutekeleza amri ya Allah (S.W)
C. Swala ndio kiingilio cha mtu katika Uislamu
D. Swala huimarisha afya na kuleta umoja.

(viii) Ipi si hukmu ya Nuun Saakina na Tanwin kati ya hizi zifuatazo?

A. Iqbaal
B. Idh – haar
C. Ikhfaau
D. Idghaam

(ix) Sembe aliwaeleza wanafunzi wenzake adabu za kusoma Qur’an, lakini alikosea hoja moja katika maelezo yake. Bainisha hoja iliyokosewa na mwanafunzi huyo.
A. Kuhakikisha msomaji anazingatia aya zinazotaja adhabu pekee
B. Kutekeleza maamrisho yake na kuacha makatazo yake
C. Msomaji wa Qur’an awe twahara kwa mujibu wa sharia

D. Kuanza kusoma Qur’an kwa kumlaani sheitwani.

(x) Sentensi ipi kati ya zifuatazo inaonesha tofauti kati ya Sunnah na Hadithi?
A. Hadithi ni lazima kuifuata ambapo Sunnah ni hiyari
B. Sunnah zipo chache na Hadithi ni nyingi
C. Hadithi ni vitendo na Sunnah ni nadharia
D. Sunnah ni vitendo na Hadithi ni nadharia.

2. Oanisha swala za sunnah kutoka orodha B na nyakati za kuswali kila sunna kutoka orodha A, kisha uandike herufi ya jibu katika sehemu iliyotengwa.

| **Orodha A** | **Orodha B** |
|---|---|
| (i) Hutekelezwa mara tu baada ya kuingia msikitini. | A. Tahajudi |
| (ii) Hutekelezwa baada ya swala ya isha kabla ya kuingia swala ya asubuhi. | B. Witri |
| (iii) Hutekelezwa usiku wa manane mara baada ya kuamka kutoka usingizini. | C. Dhuhaa |
| (iv) Hutekelezwa kabla ya swala ya faradhi kuswaliwa na ambayo inaambatana na swala husika ya faradhi. | D. Istikhara |
| (v) Hutekelezwa baada ya jua kuchomoza na kupanda juu kiasi cha mita tatu. | E. Qabliyyah |
| | F. Swalatul – istisqaa |
| | G. Tahiyatul – masjid. |

Majibu

| Orodha A | (i) | (ii) | (iii) | (iv) | (v) |
|---|---|---|---|---|---|
| Orodha B | | | | | |

**SEHEMU B (Alama 70)**

Jibu maswali yote katika sehemu hii

3. Kuna wanaodai kwamba Mwenyezi Mungu hayupo kwa kushindwa kumtambua. Fafanua njia nne zitakazowasaidia kumtambua.

(i) ______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

(ii) ______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

(iii) ______________________________________________
______________________________________________
______________________________________________

(iv) ______________________________________________
______________________________________________
______________________________________________

4. Katika kipindi cha somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu mlijifunza kuhusu fani ya fiqhi. Wafafanulie wanafunzi wenzako matapo ya fani hiyo huku ukiwatolea mifano ya wazi kwa kila tapo.

(i) ______________________________________________
______________________________________________
______________________________________________

(ii) ______________________________________________
______________________________________________
______________________________________________

5. Qur'ani ni kitabu kilichoteremshwa polepole kulingana na matukio, na uteremshwaji huu ulifanyika kwa sababu maalumu. Bainisha sababu nne kuu miongoni mwa hizo.

(i) ______________________________________________
______________________________________________

(ii) ______________________________________________
______________________________________________

(iii) ______________________________________________
______________________________________________

(iv) ______________________________________________
______________________________________________

6. Waislamu ya kijiji cha Nyamidaho ni wafuasi wa kweli wa Mtume Muhammad (S.A.W). Bainisha mambo manne yanayoonesha mwenendo wa Waislamu hao katika maisha yao ya kila siku.

(i) ______________________________________________
______________________________________________

(ii) ______________________________________________
______________________________________________

(iii) ______________________________________________
______________________________________________

(iv) ______________________________

7. Toa maelezo mafupi ili kuwapa elimu wanafunzi wenzako juu ya mambo manne anayotakiwa kufanyiwa mtu mara tu baada ya kufa.
   (i) ______________________________
   (ii) ______________________________
   (iii) ______________________________
   (iv) ______________________________

8. Onesha tofauti nne zilizopo kati ya swala ya maiti na swala ya kawaida.
   (i) ______________________________
   (ii) ______________________________
   (iii) ______________________________
   (iv) ______________________________

9. Fafanua dhana zifuatazo juu ya historia kwa mtazamo wa Uislamu.
   (i) Maana ya historia.
   ______________________________
   (ii) Asili ya mwanadamu.
   ______________________________
   (iii) Lengo la kuumbwa mwanadamu.
   ______________________________
   (iv) Lengo la kuumbwa ulimwengu na vyote vilivyomo.
   (v) ______________________________
   (vi) Hatma ya mwanadamu.
   ______________________________

**SEHEMU C (Alama 15)**

Jibu swali la **Insha** katika sehemu hii

10. Ibada ya Zakat na Sadakat ni ibada ambazo lengo lake linafanana kwa kiasi kikubwa. Pamoja na hilo kuna baadhi ya vipengele ambavyo vinazitofautisha ibada hizi. Tumia hoja tano kufafanua tofauti hizo.